

# Uzuiaji wa Maambukizi katika Utunzaji wa Vidonda

## Usafi wa Mikono

- **Kabla ya** kutangamana na mteja wa kwanza au mazingira ya mteja
- **Kabla ya** kuondoa bendeji ya kidonda na kabla ya kuweka bendeji safi.
- **Kabla ya** kuvaa glavu
- **Baada ya** hatari ya kugusa majimaji ya mwili
- **Baada ya** kutangamana na mteja au mazingira ya mteja
- **Baada ya** kuondoa glavu

## Vifaa vya Kujikinga (PPE)

- Vaa glavu wakati wa hatua zote za utunzaji wa vidonda ikiwa ni pamoja na wakati wa kufunga bendeji mpya.
- Vaa barakoa na kinga ya macho ikiwa kuna uwezekano wowote wa kutapanyika
- Vaa gauni jipya ili kuzuia kutangamana na mteja au kitanda cha mteja kila unapobadilisha bendeji.

## Zana/ Vifaa

- Zana za utunzaji wa vidonda maalum kwa kila mteja zinahitaji kuangamizwa viini baada ya utunzaji wa vidonda kukamilika, kulingana na maagizo ya watengenezaji.
- Hifadhi zana/vifaa inavyofaa hadi utakapobadilisha bendeji tena kulingana na miongozo ya kituo.

## Vifaa vya kutumia mara moja

- Lihamu na krimu zinapaswa kutengewa mteja mmoja.
- Ikiwa unatoa dawa nyingi, usafi wa mikono na glovu zinapaswa kutumiwa kuweka katika kikombe cha dawa ili kuzuia bakteria kuingia kwenye chombo.
- Vifaa vya bendeji vinapaswa kutengewa kidonda kimoja na si vingi.

**Vidonda ambavyo havijafungwa vinatoa njia kwa viini kuingia na kusambaa kwenye mwili mzima.**

## Je, ulijua ?

- Dumisha utengano baina ya zana safi na chafu ili kuzuia uchafuzi mbaya.
- Kifaa chochote kinachoweza kutupwa ambacho hakijatumiwa kinachoingia katika eneo la utunzaji wa mgonjwa/mkazi kinapaswa kusalia kutengewa mgonjwa/mkazi huyo au kitupwe.